# Shared reading: the key ingredient for improving students' educational outcomes

## A professional learning course for primary and secondary school teachers

'Reading aloud with children is known to be the single most important activity for building the knowledge and skills they will eventually require for learning to read' (Jager Adams, 2013).

Mshauri Education

By Catherine Duffett
(Bsc(Hons), DipEd, Med(Teachlib), GradCertEd(LitEd)
Orton-Gillingham Classroom Educator Level OGCE/OGA

Imetafsiriwa na Asante Skuli

info@mshauried.org

www.mshauried.org

# Kuhusu Mwandishi

Catherine Duffett ana zaidi ya miaka ishirini ya uzoefu katika ufundishaji nchini Australia. Amehudumu katika miji ya Hobart, Darwin na Alice Springs, katika shule za umma na binafsi zenye utofauti mpana wa kitamaduni. Aidha, ana uzoefu wa zaidi ya miaka kumi kama *mwalimu wa maktaba* katika shule za msingi na sekondari, na kwa sasa anafanya kazi kama *mwalimu wa maktaba* katika shule ya msingi. Mwaka 2013 alitunukiwa tuzo ya **Tasmanian Teacher Librarian of the Year**. Catherine pia amewahi kufundisha masomo ya Sayansi na Hisabati kwa wanafunzi wa sekondari na ni mwalimu mwenye sifa za kitaalamu katika ufundishaji wa usomaji.

Catherine ana ari na dhamira ya kutumia mbinu zenye ushahidi wa kitaaluma ili kuboresha fursa za kielimu kwa watoto, hususan wale wanaotoka katika mazingira yenye changamoto, pamoja na kushirikisha utaalamu na maarifa yake na wadau wengine.

Kwa sasa, Catherine anajitolea muda wake kama mshauri wa elimu kwa asasi zisizo za kiserikali katika nchi zinazoendelea, akifanya kazi ya kuboresha matokeo ya kielimu kwa watoto kutoka katika mazingira duni. Jina la biashara yake, *Mshauri Education*, alipewa na marafiki zake wa Kitanzania. Neno *mshauri* kwa Kiingereza linamaanisha “advisor” au “consultant.”

# Jinsi ya Kutumia Kozi Hii

Ingawa kozi hii inaweza kutumiwa na walimu wanaojifunza binafsi kwa ajili ya maendeleo ya kitaaluma, inapendekezwa kwa kiwango kikubwa kwamba, pale inapowezekana, walimu wajihusishe na ujifunzaji wa pamoja. Mtindo huu unakuza majadiliano ya kina, tafakuri, na uelewa mpana wa tafiti zilizowasilishwa. Kwa madhumuni haya, kozi imegawanywa katika vitengo mbalimbali vinavyoambatana na maswali ya mjadala kwa walimu kuyajadili na kutafakari.

Mbinu ya *Final Word Protocol* (Faddis, h.k.) ni miongoni mwa mbinu bora za kuendesha mafunzo ya kitaaluma, kwa kuwa inakuza ushirikiano, fikra za kina na uchambuzi wa maandishi. Mbinu hii hutekelezwa kama ifuatavyo:

1. Walimu hupangwa katika makundi ya watu watatu au wanne, na kila mshiriki kupewa utambulisho wa herufi A, B, C au D.
2. Kila mwalimu husoma maandishi au sehemu ya maandishi, kuchagua nukuu au kifungu kilichomgusa, na kuiandika kwenye karatasi maalumu .
3. Mwalimu A husoma kwa sauti nukuu yake kwa kundi, kisha hutumia dakika tatu kueleza sababu ya uchaguzi wake na umuhimu wa nukuu hiyo.
4. Walimu B, C na D hutumia dakika moja kila mmoja kutoa maoni yao kuhusu hoja ya Mwalimu A. Wanaweza kuwasilisha mtazamo wao binafsi, kufafanua, au kuhoji misingi ya hoja ya Mwalimu A.
5. Mwalimu A hutoa muhtasari wa michango yote iliyotolewa, kisha kueleza ikiwa maoni ya wenzake yamebadilisha mitazamo yake kuhusu mada hiyo.
6. Mwalimu B huwasilisha nukuu aliyoichagua na sababu ya umuhimu wake, huku akibainisha ikiwa mjadala uliotokea kuhusu nukuu ya Mwalimu A umeathiri mtazamo wake. Mchakato huo hurudiwa kwa kufuata mpangilio huo huo, ambapo Waalimu A, C na D hujibu mawazo ya Mwalimu B.
7. Hatimaye, Walimu C na D hupata nafasi yao ya kushiriki sehemu za maandishi zilizowaathiri au kuwagusa zaidi.
8. Baada ya kukamilika kwa mijadala katika makundi madogo, makundi yote huungana ili kubadilishana mawazo na mitazamo yao.

9. Ili kuimarisha zaidi ujifunzaji, muda maalumu hutengwa kwa ajili ya walimu kutafakari kwa pamoja na wenzao, kuandika katika daftari la tafakuri (*journal*), au kupanga hatua watakazochukua wakitumia uelewa mpya walioupata.

## Shukurani

Shukrani za dhati kwa Brian Stace kwa kazi yake ya uhariri makini, na kwa wote waliofanya uhakiki wa kitaalamu  wa kozi hii.

**Hakimiliki © 2024 Mshauri Education**

Kazi hii imetolewa chini ya leseni ya **Creative Commons Attribution–NonCommercial 4.0 International Licence**. Ili kuona nakala ya leseni hii, tembelea: http://creativecommons.org/licenses/by-nc/4.0/.

Unaruhusiwa kushiriki, kunakili na kusambaza kazi hii katika mfumo wowote au kupitia njia yoyote, kwa kuzingatia masharti yafuatayo:

- **Utambuzi wa Mmiliki:** Ni lazima utoe sifa stahiki kwa mwandishi/wandishi wa asili, utoe kiungo cha leseni, na uonyeshe iwapo mabadiliko yoyote yamefanywa kwenye kazi.
- **Matumizi Yasiyo ya Kibiashara :** Huwezi kutumia kazi hii kwa madhumuni ya kibiashara.

  Kwa matumizi mengine yoyote, tafadhali wasiliana na Mshauri Education

# 1

# Kwanini Kusoma kwa Sauti kwa Wanafunzi?

**Utangulizi**

Kusoma kwa sauti kwa wanafunzi ni mojawapo ya mikakati yenye ufanisi mkubwa ambayo mwalimu anaweza kuitumia ili kujenga maarifa na kukuza stadi za kusoma na kuandika. Ingawa wanafunzi bado wanahitaji fursa za kutosha za kushiriki katika usomaji wa kujitegemea, kusoma kwa sauti mara kwa mara aina mbalimbali za matini kwa wanafunzi kunaweza kuwa sehemu muhimu na yenye mvuto katika muda wa ufundishaji.

Kozi hii imeandaliwa mahsusi kwa ajili ya walimu katika nchi zinazoendelea, ambako upatikanaji wa rasilimali za usomaji kwa matumizi ya wanafunzi ni mdogo. Kwa kuhakikisha kuwa usomaji wa sauti kwa wanafunzi unafanywa mara kwa mara na unajumuisha mikakati inayotokana na ushahidi wa utafiti, walimu wanaweza kuboresha matokeo ya kielimu ya wanafunzi wao.

Sehemu kubwa ya taarifa zinazotolewa katika kozi hii kuhusu ufahamu wa kusoma pia zinatumika pale ambapo wanafunzi wanasoma matini wao wenyewe. Kozi hii inafaa kwa walimu wa elimu ya awali, elimu ya msingi na elimu ya sekondari, na tafiti pamoja na mikakati iliyoelezwa ndani ya kozi hii inafaa kwa wanafunzi wanaojifunza lugha yoyote.

**Kwanini kusoma kwa sauti kwa wanafunzi?**

Kusoma mara kwa mara kwa sauti kwa wanafunzi ni mbinu yenye ufanisi mkubwa ambayo inaathiri kwa njia chanya mafanikio ya kielimu ya wanafunzi kwa njia zifuatazo:

1. *Huchangia kuongezeka kwa mafanikio ya juu ya kitaaluma.*
   Utafiti uliofanywa na Shirika la Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo (Organisation for Economic Co-operation and Development (OECD)) ulihitimisha kuwa kuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya marudio ya kusomewa kwa sauti kwa watoto wadogo na kiwango cha mafanikio yao ya baadaye ya kitaaluma. Watafiti walibainisha kuwa watoto waliokuwa wakisomewa kwa sauti mara kwa mara na wazazi wao wakiwa katika Darasa la Kwanza walipata alama za juu zaidi katika Tathmini ya Kimataifa ya Wanafunzi (Programme for International Student Assessment (PISA)) walipofikia umri wa miaka 15, bila kuathiriwa na tofauti za hali ya kijamii na kiuchumi za wanafunzi hao (Anderson, 2015).

2. *Kuongeza ushiriki wa wanafunzi.*
   Albright na Ariail (2005) waligundua kuwa kusoma kwa sauti kwa wanafunzi wa Miaka ya 7 na 8 kunasababisha ongezeko la ushiriki wao katika masomo.

3. *Kufahamisha maandishi changamano.*
   Kusoma kwa sauti kunawawezesha wanafunzi kufikia maandishi ambayo hawawezi kusoma wenyewe, na hivyo kuwasaidia kuwa wasomaji na waandishi bora zaidi (Lemov, Driggs na Woolway, 2016).

4. *Kuumba mfano wa mbinu za uelewa.*
   Wakati wa kusoma kwa sauti, walimu wanaweza kuelezea fikra zao kuhusu maandishi, na hivyo

kuonyesha kwa wanafunzi jinsi ya kuelewa maandishi (Furman, 2019).

5*. Kufahamisha msamiati mpya.*
Inatoa nafasi ya kuwafahamisha wanafunzi msamiati na mawazo mapya, na kuwasaidia kuelewa kuwa lugha ya maandishi ni tofauti na lugha ya mdomo (Hedrick na Pearish, 2003 kama ilivyotajwa na Fisher et al., 2004).

6*. Kuumba mfano wa usomaji wenye ufasaha.*
Kusoma kwa sauti kunatoa fursa ya kuonyesha usomaji wenye ufasaha kwa kusoma kwa hisia na mvuto. Kusoma maandishi yasiyo ya kubuni na hadithi za kubuni kunawawezesha wanafunzi kutambua kuwa maandishi ya nonfiction yana mpangilio tofauti (Dougherty Stahl, Flanigan na Mckenna, 2020; Lemov, Driggs na Woolway, 2016).

## Kamba ya Kusoma

Kamba ya Kusoma (Mchoro 1) ni fumbo inayotumika kuelezea kinachohitajika ili kupata ujuzi wa kusoma kwa ustadi. Kulingana na mfano huu, kusoma kwa ufanisi kunahitaji mtu kumiliki ujuzi 6 tofauti, ambazo zinawakilishwa na nyuzi za kamba. Mfano huu pia unaonyesha kuwa kuna nyuzi kuu mbili zinazowakilisha ufahamu wa lugha na utambuzi wa maneno (Dougherty Stahl, Flanigan na Mckenna, 2020). Kama kozi hii itakavyothibitisha, kusoma kwa sauti kwa wanafunzi kunaathiri kwa nguvu nyanja mbalimbali za ufahamu wa lugha.


**Tafakari na Jadili**

1. Kwa kiwango gani kwa sasa unasoma kwa sauti pamoja na wanafunzi wako?

2. Ni kwa njia zipi unaamini wanafunzi wako wangeweza kufaidika zaidi iwapo ungejumuisha vipindi vya kusoma kwa sauti kwa wingi zaidi katika ufundishaji wako?

3. Kuandaa tukio la usomaji linalojumuisha kusoma kwa sauti kwa wanafunzi ni njia yenye mvuto ya kukuza na kuhamasisha fasihi. Kiambatisho cha 1 kinatoa maelezo ya aina mbalimbali za matukio yanayoweza kutoa msukumo kwa shule kuunda matukio yao wenyewe.

4. Je, kuna tukio lolote la usomaji lililoelezwa katika Kiambatisho hiki ambalo linaweza kufaa kwa shule yako?




**Mchoro 1: Kamba ya Kusoma ya Scarborough**

**SCARBOROUGH'S READING ROPE TRANSLATED.**

**TAFSIRI YA KAMBA YA KUSOMEA YA SCARBOROUGH**

| | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **ENG** | **LANGUAGE COMPREHENSION** | | | | | | | | | | |
| **SWA** | **UFAHAMU WA LUGHA** | | | | | | | | | | |
| **ENG** | Background knowledge | | Vocabulary | | | Language structures | | verbal reasoning | | Literacy knowledge | |
| **SWA** | **Ufahamu wa Awali** | | **Msamiati** | | | **Miundo ya Lugha** | | **Mantiki ya Kimsamiati** | | **Maarifa ya Kusoma na Kuandika** | |
| **ENG** | Facts | Concepts | Breadth | precision | links | Syntax | semantics | Inference | metaphor | print concepts | Genres |
| **SWA** | **uhakika** | **Dhana** | **Upana** | **Usahihi** | **Uhusiano** | **Sentensi** | **Semantiki** | **Hitimisho** | **Methali** | **Mikondo ya Chapisho** | **Aina za Maandishi** |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **ENG** | **WORD RECOGNITION** | | | | |
| **SWA** | **UTAMBUZI WA MANENO** | | | | |
| **ENG** | **Phonological awareness** | | **DECODING** | | **SIGHT RECOGNITION (of familiar words)** |
| **SWA** | **Uelewa wa fonolojia** | | **Usimbuaji wa maneno** | | **Utambuzi wa maneno kwa mtazamo** ( Wa maneno yanayofahamika) |
| **ENG** | Syllables | phonemes | Alphabetic principle | spelling-sound correspondences | |
| **SWA** | **Silabi** | **Fonimu** | **Kanunu ya kialfabeti** | **Ulinganifu kati ya Herufi na Sauti** | |

## 2 Kujenga Uelewa wa Awali / Kujenga Maarifa ya Msingi

### Umuhimu wa Maarifa ya Awali

Maarifa ya awali yanahusiana na uzoefu mbalimbali ambao msomaji amepata na ambao humwezesha kuelewa maandishi (Brody, 2001 kama ilivyotajwa na Lewis Hennessy, 2021). Uwepo wa maarifa haya ni muhimu kwa ufanisi wa kujifunza nyenzo mpya, kwani mtu hutegemea uzoefu wake wa awali na maarifa aliyokuwa nayo ili kutoa maana na kuelewa maarifa mapya (The National Research Council, 2000 kama ilivyotajwa na Lewis Hennessy, 2021). Kielelezo cha 1 kinaonesha kwamba maarifa ya awali ni mojawapo ya ujuzi sita muhimu unaochangia kwa kiasi kikubwa katika ufahamu wa lugha.

### Athari za Umaskini kwa Maarifa ya Awali

Kwa bahati mbaya, wanafunzi kutoka familia zisizo na elimu ya kutosha wana uwezekano mdogo wa kuwa na maarifa ya awali ikilinganishwa na wale kutoka kwa familia zenye hali ya juu ya kijamii na kiuchumi. Hii ni kutokana na upungufu wa rasilimali za kifedha zinazowezesha kununua vitabu na kupata uzoefu wa kielimu unaosaidia kujenga maarifa. Tofauti ya maarifa inayoonekana kati ya watoto kutoka familia zisizo na rasilimali na wale kutoka familia zilizo na rasilimali nyingi huongezeka kadri wanafunzi wanavyoendelea katika masomo yao (Wexler, 2019).

Hata hivyo, kwa kuandaa mazingira ya ujifunzaji yenye utajiri wa fasihi, ambapo watoto wanapata fursa ya kukutana na maandiko yenye changamoto ya juu ya kifikra na kiisimu, walimu wanaweza kuchangia kwa kiasi kikubwa kupunguza na hatimaye kuziba pengo hili la maarifa (Furman, 2019).

### Kusoma kwa Sauti Ili Kupunguza Pengo la Maarifa

Uelewa wa kusikiliza wa wanafunzi kwa ujumla huwa juu zaidi kuliko uelewa wao wa kusoma. Kwa hivyo, kusoma kwa sauti makala za kisayansi na vyanzo vya awali vinavyobeba dhana, sarufi, na msamiati ulio juu ya uwezo wa msomaji kusoma peke yake ni mkakati muhimu wa kupunguza pengo la maarifa (Lemov, Driggs, na Woolway, 2016).

Kusoma kwa sauti maandishi kama haya husaidia kuweka msingi kwa wanafunzi kusoma maandishi rahisi zaidi kuhusu mada ile ile. (Lemov, Driggs, na Woolway, 2016).

Kifaa cha flash kinachokuambatana na mpango huu wa mafunzo kina nyenzo mbalimbali zinazofaa kutumika kwa mkakati huu wa kusoma kwa sauti.

**Fikiria na Jadili:**

1. Jadili na wenzako njia za kujenga mkusanyiko wa nyenzo zinazoweza kusomewa kwa sauti kwa wanafunzi. Kwa mfano, je, magazeti, majarida, au vyanzo vingine vinaweza kutumika kwa madhumuni haya ?

2. Pitia nyenzo zilizotolewa kwenye flash drive. Ni maandishi gani unaweza kuyachanganya kwenye kitengo chako kijacho ili kuimarisha maarifa ya awali ya wanafunzi?

3

# Kufundisha Msamiati

### Kwanini Kufundisha Msamiati?

Kielelezo cha 1 kamba ya kusoma kinaonyesha kuwa ujuzi wa msamiati ni mchango muhimu katika kufanikisha uelewa wa maandishi. Watoto kutoka familia zisizo na rasilimali nyingi kwa ujumla huanza shule wakiwa na misamiati michache ukilinganisha na watoto kutoka familia zenye hali ya juu ya kijamii na kiuchumi. Kwa bahati mbaya, kama ilivyo kwa maarifa ya awali, tofauti hii katika ujuzi wa msamiati inaendelea kuwepo au hata kuongezeka kadri watoto wanavyoendelea wakiwa mashuleni (Beck, McKeown, na Kucan, 2013).

Hata hivyo, walimu wanaweza kuchangia kupunguza pengo hili kwa njia ya ufundishaji wa msamiati kwa uwazi sambamba na kusoma maandishi yaliyojaa msamiati kwa wanafunzi, jambo linalowapa uzoefu halisi na wa kufurahisha wa kujifunza.

### Mikakati ya Kufundisha Msamiati

Wakati wa kusoma maandishi kwa sauti, lengo kuu ni kuhakikisha kuwa wanafunzi wanaweza kutoa maana kutokana na maandishi, badala ya kujifunza kwa kina maneno binafsi. Kwa hivyo, walimu wanapaswa kupunguza maelezo ya kina kuhusu msamiati na badala yake kutoa ufafanuzi mfupi wa maneno mawili hadi matatu ambayo hayaeleweki pale yanapojitokeza katika maandishi (Beck, McKeown, na Kucan, 2013). Ikiwa maneno mengi sana yatajadiliwa, kuna hatari kwamba hili linaweza kuathiri uelewa wa wanafunzi kwa njia hasi (Beck, McKeown, na Kucan, 2013).

Baada ya kusoma, lengo hubadilika kuwa ukuaji wa msamiati, na maneno yoyote ya ziada yanayohitaji ufafanuzi yanaweza kujadiliwa na kuingizwa katika shughuli za kufuata ili kuthibitisha maana ya maneno hayo (Beck, McKeown, na Kucan, 2013).

### Rutini ya Kifundisho ya Kufundisha Msamiati

Kindle (2009, ikitolewa na Lewis Hennessy, 2021) anapendekeza rutini ifuatayo ya kifundisho ya kufundisha msamiati baada ya maandiko kusomwa:

1. Chagua msamiati kutoka Kenya maandiko ambao unahitaji ufafanuzi.
2. Wakati wa kusoma kwa sauti, toa ufafanuzi, neno lenye maana sawa, picha, au swali ili kueleza maana ya maneno yaliyochaguliwa kadiri yanavyotokea katika maandiko.
3. Endelea kuingiza msamiati huu katika majadiliano na kazi za uandishi.

### Kutumia Vitabu vya Lugha Mbili Kufundisha Msamiati

Maneno yanayofanana katika lugha mbili yanayofanana kwa maana na uchapaji huitwa *cognates (kwa Kiingereza)*. Beck, McKeown na Kucan, (2013) wanapendekeza kuwa kusaidia wanafunzi kutambua ulinganifu kati ya maneno katika lugha zote mbili kunaweza kukuza uelewa wao wa lugha ya Kiingereza.

Utafiti uliofanywa kwa wazungumzaji wa asili wa Kihispania unaonyesha kuwa wakati wanafunzi wanaweza

kutambua *cognates* hizi kwa Kiingereza na Kihispania, uelewa wao wa Kiingereza unaimarika. Inaonekana kuwa mantiki hii inaweza kutumika pia kwa lugha nyingine za asili.

Hivyo basi, vitabu vya lugha mbili vinaonekana kuwa chombo chenye manufaa katika kusaidia watoto kuchambua *cognates*, na hivyo kukuza uelewa wao wa lugha ya Kiingereza.

García, Sacco na Guerrero-Arias (2020) wanapendekeza kwamba walimu wanaweza kusaidia wanafunzi kwa:

- Kutambua na kujadili maneno yanayofanana (cognates) yanayojitokeza katika maandiko kwa uwazi.
- Kuwataka wanafunzi kuweka kumbukumbu ya maandishi ya maneno yanayofanana wanayokutana nayo, ili maneno hayo yaweze kurejelezwa mara kwa mara.
- Kuonesha mfano wa jinsi ya kuhakiki kama neno linalofanana limechaguliwa kwa usahihi, kwa kulinganya kwenye sentensi na kuona kama maana yake inafaa.

**Fikiria na Jadili:**

1. Pitia rasilimali zilizomo kwenye flash drive iliyoambatanishwa.
2. Chagua maandiko yanayofaa kusomwa kwa sauti katika somo lijalo.
3. Tambua msamiati unaostahili kufundishwa na panga ufundishaji wa wazi wa msamiati utakaofanyika baada ya maandiko kusomwa kwa sauti.

# 4 Kufundisha miundo ya lugha na maarifa ya usomaji na uandishi

## Miundo ya Lugha na Nafasi Yake Katika Ufafanuzi wa Maandishi

Wasomaji hodari wana uelewa wa jinsi lugha inavyoundwa na hutumia maarifa hayo kuunda maana kutokana na maandishi. Sintaksia hurejelea nafasi na jukumu la maneno ndani ya sentensi, kwa mfano iwapo neno ni nomino, kitenzi au kivumishi. Sintaksia ndiyo hutoa utaratibu wa kuyaainisha aina mbalimbali za maneno, jambo linalowezesha uhifadhi wake katika kumbukumbu na urejeshaji wake wakati unahitajika.Katika lugha ya Kiingereza, sentensi kwa kawaida hupangwa kwa mtiririko ambapo kiima (ambacho sentensi inamhusu), kinachojulikana pia kama mtenda, hufuatiwa na kiarifu, yaani kitenzi kinachoonesha kitendo cha kiima (Kambach na Mesmer, 2024).

Uelewa wa miundo ya lugha ni muhimu katika ufahamu, kwani humwezesha mwanafunzi siyo tu kuelewa na kuunganisha sentensi, bali pia kufahamu wazo kuu la maandishi (Kintsch, 2018 alinukuliwa na Kambach na Mesmer, 2024).

## Mikakati ya Kufundisha Sintaksia


Utoaji wa fursa endelevu kwa wanafunzi kusoma au kusomewa maandishi yenye miundo tata ya kisarufi umebainika kuwa njia mahsusi na thabiti katika kuwajengea uwezo wa kuelewa dhana ya sintaksia kwa kiwango cha juu (Lemov, Driggs na Woolway, 2016). Baada ya usomaji huo, ni vyema kufuatiwa na maswali ya kina yanayowataka wanafunzi kuchunguza na kuchanganua maandishi kwa mujibu wa mpangilio wake wa kisintaksia, hatua ambayo imeainishwa kuwa mbinu iliyo na tija katika ufundishaji (Lewis Hennessy, 2021).

*Mkakati wa wazo kuu na Maelezo ya Ziada*

Ili watoto waweze kubaini wazo kuu katika maandishi, awali ni muhimu wawe na uwezo wa kutambua wazo kuu ndani ya sentensi moja au ndani ya kikundi cha sentensi mbili hadi tatu (Kambach na Mesmer, 2024. Mkakati wa wazxo kuu na maelezo ya ziada umebuniwa mahsusi kufanikisha lengo hii kwa njia iliyo na muundo na mpangilio, hususan kwa wasomaji wanaoanza, kwa kuwa unawezesha kutofautisha kati ya wazo kuu na taarifa za ziada zinazozielezea au kulipanua (Kambach na Mesmer, 2024). Kabla ya kuanza mchakato wa usomaji wa maandishi kwa sauti, mwalimu hupaswa kutambua sentensi ambazo haziakisi muundo wa kawaida wa kisarufi wa mtenda kitenzi. Sentensi hizo huchaguliwa kwa ajili ya ufundishaji mahsusi, ulio wazi na wenye lengo la kukuza uelewa wa wanafunzi kuhusu tofauti za miundo ya kisarufi katika maandishi.

Baada ya kusomewa maandishi, wanafunzi hutakiwa kubaini wazo kuu lililomo katika sentensi, yaani sehemu inayojumuisha mtenda na kitendo , pamoja na taarifa za ziada ambazo si za msingi katika kufanikisha uelewa wa wazo hilo kuu (Kambach na Mesmer, 2024). Kwa mfano, tukilitumia sentensi ifuatayo: *“Kwa msisimko, John alikwenda kuchunguza jiji jipya,”* wanafunzi huongozwa awali kutambua kwamba *John* ndiye mtenda wa sentensi, na kwamba kitendo anachokifanya ni *kuchunguza jiji jipya*.

Baadaye, wanafunzi hulenga kubainisha taarifa za ziada ambazo si muhimu kwa uelewa wa msingi wa sentensi, ambazo katika mfano huu ni *“Kwa msisimko.”* Kambach na Mesmer (2024) wanashauri kutumia vielelezo vinavyoonyesha wazo kuu mahsusi kwa watoto, ili kuongeza usaidizi wa kimkakati katika mchakato wa ujifunzaji, kama inavyoonyeshwa kwenye Mchoro wa 2.




**Kielelezo 2: Mchoro unaoonyesha *Mawazo Makuu (Big Ideas) na mkakati wa Extra* kwa sentensi*: Kwa shauku, John alikwenda kuchunguza mji mpya.***

Mara watoto wanapolizoea mkakati huu, wanaweza kutumia mbinu hiyo hiyo kuchanganua sentensi mbili au tatu zilizounganishwa (Kambach na Mesmer, 2024) kabla ya kuendelea kuchanganua vipande virefu zaidi vya maandishi.

## Matumizi ya vielelezo vya upangaji mawazo

Kuwauliza wanafunzi kujibu maandishi kwa maswali kama *nani?*, *nini?*, *wapi?*, *lini?*, *kwa nini?* na *vipi?* ni mkakati mwingine unaotumika kuchanganua maandishi kwa kuzingatia sintaksia yake. Endapo itahitajika, walimu wanaweza kufanya mbinu hii iwe wazi zaidi kwa kutumia vielelezo vya upangaji mawazo pamoja na wanafunzi, kama inavyooneshwa katika Kielelezo cha 3.

| | Maandishi yanasema kuwa… | Ninajua kutokana na maarifa yangu ya awali kuwa… | Ninahitimisha kuwa… |
|---|---|---|---|
| Nani? | | | |
| Nini? | | | |
| Wapi? | | | |
| Lini? | | | |
| Kwanini? | | | |
| Kivipi? | | | |

**Kielelezo 3: upangaji mawazo (graphic organisers) cha kusaidia ufundishaji wa sintaksia (Lewis Hennessy, 2021).**

## Maarifa ya Ujuzi wa Kusoma na Kuandika

Maarifa ya ujuzi wa kusoma na kuandika yanarejelea:

*Dhana za maandishi* - kwa mfano, uelewa kwamba maneno husomwa kutoka kushoto kwenda kulia, kwamba kuna nafasi kati ya maneno, na kwamba maneno huundwa na herufi (Lewis Hennessy, 2021). Ili kusaidia watoto kuelewa dhana za maandishi, mwalimu anaweza kuuliza maswali kama vile: *Je, unaweza kuonyesha kichwa cha habari kwenye jalada?* au *Nionyeshe ni wapi ninapaswa kuanza kusoma katika ukurasa huu?* Mwalimu pia anaweza kutumia viashiria visivyo vya maneno, kama vile kufuatilia maneno kwa kidole wakati wa kusoma (Lane na Wright, 2007).

*Maarifa ya aina mbalimbali za tungo za uandishi* - kwa mfano, ripoti za taarifa, maandishi ya ushawishi, na masimulizi; aina hizi hujengwa kwa miundo tofauti kwa kuwa zina malengo tofauti.

Wakati wa kusoma kwa sauti, walimu wanaweza kuimarisha maarifa ya watoto kuhusu ujuzi wa kusoma na kuandika kwa kufikiri kwa sauti wanaposoma. Kwa mfano, wakati wa kusoma kwa sauti maandishi yasiyo ya kubuni , mwalimu anaweza kuonesha jinsi ya kupata taarifa kwa kutumia vipengele vya maandishi kama vile vichwa vya habari, maelezo ya picha, na kurasa za yaliyomo. Vilevile, wakati wa kusoma kwa sauti simulizi, mwalimu anaweza kuchochea majadiliano kuhusu mwanzo wa hadithi, mgogoro, na ufumbuzi ili kuwasaidia watoto kuelewa muundo wa msingi wa simulizi (Lane na Wright, 2007).

**Tafakari na Jadili**

1. Chagua maandishi (ya kubuni au yasiyo ya kubuni) yatakayosaidia kufikia malengo ya ujifunzaji kwa somo lijalo.

2. Ni vipengele gani vya maandishi vinastahili kufundishwa?

3. Bainisha miundo yoyote ya lugha unayotarajia wanafunzi wataona kuwa changamoto kuielewa. Unapanga vipi kuwaunga mkono wanafunzi katika kuelewa sentensi hizo?

4. Ni vipengele vipi vya aina mahususi ya maandishi uliyochagua vinavyostahili kujadiliwa pamoja na wanafunzi wako?

# 5 Kujenga ujuzi wa wanafunzi katika hoja za kimaelezo

**Ujuzi wa hoja za kimaelezo na mchango wake katika ufahamu wa maandishi**

Ujuzi wa hoja za kimaelezo hutumika pale msomaji anapohitajika kutoa hitimisho kutoka katika maandishi ili kuyafahamu. Kama inavyoonyeshwa na kamba ya kusomea (Mchoro wa 1), ujuzi huu ni wa msingi kwa usomaji wenye umahiri. Hoja za kimaelezo zinahitajika katika kupanga mfuatano wa matukio, kubainisha maana inayodokezwa na sitiari, kuunganisha taarifa mbalimbali, na kuchanganua maandishi (Kambach na Mesmer, 2024). Ingawa uchambuzi wa kina wa tafiti kuhusu ujuzi wa hoja za kimaelezo na nafasi yake katika kufanya hitimisho uko nje ya upeo wa kozi hii, ni muhimu kuelewa baadhi ya aina za kawaida za hitimisho ambazo msomaji hulazimika kufanya.

*Uchanganuzi wa ulinganifu wa karibu wa maana katika maandishi*
Haya hutokea pale msomaji anapohitajika kutoa hitimisho kutoka katika vipande vya maandishi vilivyo karibu au vinavyofuatana, kama ilivyo kwa matumizi ya viunganishi vya mshikamano, ambapo neno au kikundi cha maneno huchukua nafasi ya kingine. Mfano wa kawaida zaidi katika lugha ya Kiswahili ni viwakilishi, kama vile **mimi** na **Yule**. Wanaojifunza lugha ya Kiswahili huenda wasifuatilie ipasavyo viwakilishi hivi wanaposoma, jambo linaloweza kusababisha changamoto katika ufahamu wa maandishi (Kambach na Mesmer, 2024). Kwa mfano, katika sentensi: “Jane **a**lijiandaa kwa ajili ya kwenda shuleni. **A**likimbia kutoka nje ya mlango kwa sababu alikuwa amechelewa.” Msomaji anahitaji kutambua kuwa kiwakilishi **A** kinamrejelea Jane.

Ili kuwasaidia wanafunzi kufuatilia matumizi ya viwakilishi, mwalimu anaweza kuelekeza kwa makusudi umakini wa wanafunzi kwenye viwakilishi na namna vinavyotumika kuunda mshikamano wa maandishi. Endapo kitabu cha picha kinatumika, mwalimu anaweza pia kuelekeza umakini kwenye michoro ya wahusika wakati wa kusoma kwa sauti, ili kuwasaidia wanafunzi kufuatilia marejeo ya viwakilishi kwa usahihi (Kambach na Mesmer, 2024).

Kubadilisha neno kwa kutumia kisawe ni mfano mwingine wa kifaa cha mshikamano wa maandishi. Kwa mfano, katika sentensi zifuatazo, neno *gari* limebadilishwa na **Motokaa** katika sentensi ya pili: *“*Gari liliharibika barabarani wakati wa saa za msongamano wa magari. Kwa bahati nzuri, motokaa la kuvuta magari lilifika haraka ili kuliondoa gari lililokwama.*”*

Msomaji pia anahitaji kuelewa jinsi viunganishi vinavyotumika kuwasilisha maana. Haya ni maneno au virai vinavyoashiria uhusiano kati ya vipande tofauti vya maandishi. Kwa mfano, maneno kama Aidha huonesha kuwa taarifa ya ziada inatolewa, ilhali istilahi kama **kabla, baada** au pindi ambapo hutoa taarifa kuhusu wakati (Lewis Hennessy, 2021).

*Uchanganuzi wa ulinganifu wa jumla wa maana katika maandishi*
Hitimisho la ulinganifu wa jumla humhitaji msomaji kuamsha maarifa yake ya awali yanayohusiana na mada inayojadiliwa ili kuunganisha na kuchanganua taarifa zilizomo katika maandishi. Kwa mfano, msomaji

hutumia aina hii ya hitimisho kutambua mazingira ya hadithi, kutoa hitimisho, au kubaini mtazamo wa mwandishi (Lewis Hennessy, 2021).

## Kujenga ujuzi wa hoja za kimaelezo kwa wanafunzi

Mikakati ifuatayo inaweza kutumika kujenga ujuzi wa hoja za kimaelezo kwa wanafunzi.

*Kuuliza maswali*
Walimu wanaweza kutumia kwa makusudi usomaji wa sauti ili kujenga ujuzi wa hoja za kimaelezo kwa wanafunzi kwa kuuliza maswali ya wazi (Kambach na Mesmer, 2024). Kitengo cha 6 cha kozi hii kinatoa baadhi ya mikakati iliyothibitishwa kwa utafiti kwa ajili ya kusaidia (kuskafulidi) majadiliano na wanafunzi kuhusu maandishi kwa kutumia maswali ya aina hii.

*Kufikiri kwa sauti*
Mwalimu anaweza kuonesha namna ya kufanya hitimisho kwa kufikiri kwa sauti mbele ya wanafunzi (Lewis Hennessy, 2021).

## Vichoro vya kupanga mawazo

Vichoro vya kupanga mawazo pia vinaweza kuwasaidia wanafunzi kufanya uelekezaji wa maana kutoka katika maandishi, kama inavyooneshwa kwenye jedwali lililowasilishwa katika Kielelezo cha 4.

| swali | Maandishi yanasema nini? | Ninachokijua tayari | Kwa hiyo, nadhani … |
|---|---|---|---|
| | | | |

**Mchoro wa 4: kichoro cha kupanga mawazo kilichorekebishwa kutoka kwa Lewis Hennessy (2021) ili kusaidia wanafunzi kufanya hitimisho la ulinganifu wa jumla katika maandishi**

**Tafakari na Jadili**

1. Chagua maandishi yanayofaa kujumuishwa katika somo lijalo. Bainisha hitimisho la ulinganifu wa karibu na la ulinganifu wa jumla ambalo wanafunzi watahitaji kulifanya ili kuelewa maandishi hayo.

2. Bainisha iwapo wanafunzi watahitaji msaada ili kufanya hitimisho hilo, na aina ya msaada unaohitajika.

Ili kuimarisha ufahamu, Fisher na wenzake (2015) wanasisitiza umuhimu wa kutenga muda katika vipindi vya masomo ili kuwapa wanafunzi fursa ya kujadili maandishi baada ya kuyasoma au kuyasikiliza. Hapa chini, mifumo mitatu tofauti inaelezwa kama mbinu ya kusaidia uendeshaji wa majadiliano yenye ufanisi.

**Majadiliano Elekezi ya Maandishi kwa Kuimarisha Msamiati kwa Watoto Wadogo**

Mkakati huu unalenga kukuza ujifunzaji wa msamiati mahsusi unaotokana na maandishi fulani. Somo la majadiliano elekezi ya maandishi huanza kwa mwalimu kusoma hadithi kwa sauti, kisha kuwaongoza wanafunzi katika mjadala unaohusiana na maudhui ya maandishi hayo. Baada ya hapo, mwalimu huchagua maneno machache muhimu kutoka katika hadithi ili kuyachambua na kuyajadili kwa kina zaidi.

*Ujifunzaji wa kina wa maneno*
Yaliyochaguliwa huwa kiini kikuu cha somo. Hatua hii inaweza kujumuisha utoaji wa visawe vya maneno husika pamoja na maelezo ya matumizi yake ndani ya sentensi. Hatimaye, mjadala huelekezwa katika matumizi ya maneno hayo katika miktadha mbalimbali isiyohusiana moja kwa moja na hadithi iliyosomwa, kwa lengo la kuimarisha uelewa mpana na matumizi sahihi ya msamiati kwa watoto wadogo (Beck, McKeown na Kucan, 2013).

*Majadiliano Elekezi ya Maandishi kwa Kutumia Vitabu Vyenye Pugha Isiyo Changamano Sana*
Kutumia maandishi yaliyoandikwa katika kukuza msamiati wa wanafunzi ni mkakati wenye ufanisi mkubwa, kwa kuwa maandishi yaliyoandikwa huwa na maneno adimu zaidi ikilinganishwa na mazungumzo ya kawaida ya mdomo. Kifaa cha kumbukumbu (*flash drive*) chenye rasilimali za usomaji kinachoambatana na kozi hii kina idadi kubwa ya vitabu vya picha vya bure vilivyotayarishwa na wajitolea. Ingawa baadhi ya vitabu hivi havina lugha ya kiwango cha juu cha uchangamano kwa kuwa vimeundwa mahsusi kwa watoto kujisomea wenyewe bado vinaweza kuwa nyenzo madhubuti ya ufundishaji wa msamiati.

Majadiliano elekezi ya maandishi yanaweza kurekebishwa ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wanaendelea kujifunza msamiati muhimu. Beck, McKeown na Kucan (2013) wanapendekeza kuwa, kwa vitabu vya aina hii, walimu wanaweza kuchagua baadhi ya maneno kutoka katika maandishi na kuyatumia kufundishia visawe vyenye kiwango cha juu zaidi cha uchangamano. Kwa mfano, ikiwa mhusika anaelezewa katika maandishi kuwa *mwenye furaha*, mwalimu anaweza kutumia visawe kama *mwenye kuridhika* au *mwenye shangwe* wakati wa kumjadili mhusika huyo, hivyo kupanua na kuimarisha msamiati wa wanafunzi.

**Urejeleaji wa Maandishi**
Urejeleaji wa maandishi unafaa kwa watoto wadogo wanaoendelea kukuza dhana za msingi za uchapishaji na usomaji. Mkakati huu unahusisha kuonyesha au kujadili vipengele mbalimbali vya maandishi, kama vile kichwa cha kitabu, mwelekeo wa maandishi, au kuwauliza watoto mahali pa kuanzia kusoma katika ukurasa husika. Kupitia mbinu hii, watoto hujengewa uelewa wa kimsingi kuhusu jinsi maandishi yanavyopangwa na kusomwa.

**Uulizaji wa Kurejeshana**
Mkakati huu unahusisha wanafunzi kuuliza maswali kwa mwalimu au kwa wenzao, kwa kuwa uwezo wa kuuliza maswali yenye maana huonesha kiwango kizuri cha ufahamu wa maandishi. Uulizaji wa kurejeshana unaweza kutekelezwa kwa namna mbalimbali; hata hivyo, pendekezo mojawapo ni kuanza kwa mwanafunzi mmoja kuuliza swali, kisha mwalimu kumteua mwanafunzi mwingine kulijibu. Mwanafunzi wa pili hujaribu kujibu swali hilo, kisha huunda swali jingine kwa ajili ya mwanafunzi wa tatu, na mchakato huo huendelea kwa mpangilio huo (Dougherty Stahl, Flanigan na McKenna, 2020).

**Mienendo ya Majadiliano**
Kama ilivyoelezwa na Lemov, Driggs na Woolway (2016), utaratibu huu huwezesha aina mbalimbali za majadiliano, ikiwemo kufafanua taarifa na mawazo, kupanua hoja, kutathmini na kusintetiza. Wanafunzi hupewa vianzishi vya sentendi ili kusaidia (kuskafulidi) majadiliano yao. Baadhi ya mifano ya vianzishi vya sentensi vilivyoundwa kwa kutumia ChatGPT imewasilishwa katika Jedwali la 1 hapa chini.

| |
|---|
| **Kufafanua:**<br>● Unaweza kueleza unachomaanisha kwa …?<br>● Je, unaweza kutoa mfano wa …?<br>● Sina uhakika kama nimeelewa. Je, unaweza kufafanua …? |
| **Kupanua hoja:**<br>● Kupanuza hoja yako, ninaamini kuwa …<br>● Mfano mwingine wa hili unaweza kuwa …<br>● Zaidi ya hayo, tunaweza kuzingatia … |
| **Kutathmini:**<br>● Naona hoja yako, lakini nadhani …<br>● Wazo hili lina nguvu kwa sababu …<br>● Sina uhakika kama nakubaliana na hilo kwa sababu … |
| **Kusintetiza:**<br>● Tukiyaunganisha mawazo haya mbalimbali, inaonekana kwamba …<br>● Tukitazama mitazamo yote iliyoshirikiwa, dhamira ya pamoja ni kwamba …<br>● Tunapozingatia hoja zote mbili, inaonekana kuwa hoja kuu ni … |

**Jedwali la 1: Mifano ya vianzishi vya sentensi vya kusaidia mfumo wa Mienendo ya Majadiliano**

Mwanzoni, majadiliano yanapaswa kujikita katika maswali ya moja kwa moja (ambapo majibu hupatikana waziwazi ndaki ya maandishi), kisha hatua kwa hatua kuelekezwa kwenye maswali ya kiudhanifu/kiinferensi (ambapo wanafunzi huhitajika kuhusianisha yaliyomo katika maandishi na maarifa yao ya awali ili kutoa majibu) (Lemov, Driggs na Woolway, 2016).

## Mkakati wa Uhusiano kati ya Swali na Jibu

Uulizaji ni mkakati wenye ufanisi mkubwa katika kujenga na kuimarisha ufahamu wa wanafunzi kuhusu maandishi wanayosoma. Mkakati wa QAR (*Question-Answer Relationships*)

hutoa mfumo wa kuwawezesha wanafunzi kufikiri kwa kina na kwa mantiki kuhusu maandishi wanayoyasoma (Fisher na Frey, 2018). Mkakati huu hupanga maswali katika makundi mawili makuu: maswali ya kitabu (yaani maswali ya moja kwa moja/literal) na maswali ya fikra (yaani maswali ya kiinferensi), kama walivyoeleza Fisher na Frey (2018), na yanajumuisha:

*Maswali Yanayohusiana na Maandishi au Jibu la Moja kwa Moja*
Haya ni maswali ya kimaudhui (literal) ambapo majibu yake yanapatikana waziwazi ndani ya maandishi, kwa kawaida katika sentensi moja.

*Maswali Yanayohusiana na Maandishi au Changanua na Tafuta Taarifa*
Haya pia ni maswali ya kimaudhui, lakini majibu yake yanahitaji uchanganuzi na ujumuishaji wa taarifa kutoka katika sentensi au vipengele zaidi ya kimoja vya maandishi.

*Maswali Yanayohusiana na Ufasiri Au Mwandishi na Msomaji*
Maswali haya humtaka mwanafunzi kuunganisha taarifa zilizowasilishwa na mwandishi pamoja na maarifa yake ya awali ili kutoa majibu yenye mantiki na uhalali wa kitaaluma.

**Maswali Yanayojitegemea Kifikra – "Uelewa Binafsi"**

Maswali haya yanategemea zaidi maarifa na uzoefu wa awali wa mwanafunzi. Maandishi yanaweza kutumika kama rejea ya ziada au yasihitajike kabisa katika kujibu maswali haya (Fisher na Frey, 2018).

**Vihamasishi vya Mwalimu kwa Kufikiri kwa Sauti**

Oczkus (2012) anatoa orodha ya vihamasishi muhimu vinavyoweza kutumiwa kuchochea majadiliano kuhusu masimulizi kati ya wanafunzi wawili au zaidi. Vihamasishi hivi ni pamoja na yafuatayo:

*Kabla ya Kusoma*
- Nafikiri maandishi haya yanahusu … kwa sababu
- Tayari yananikumbusha … kwa sababu …
- Nafikiri nitajifunza … kwa sababu …

*Wakati na Baada ya Kusoma*
- Nilichanganyikiwa pale ambapo …
- Mwanzoni nilidhani …, lakini baadaye nikatambua
- Nilishtushwa na … kwa sababu …
- Hadi sasa, … limetokea …
- Hili linanikumbusha … kwa sababu …
- Jambo jipya nililojifunza ni …
- Nilipenda sehemu ambayo … kwa sababu …
- Ilikuwa (ya kuchekesha, ya kusikitisha, ya kushangaza) pale ambapo …
- Nafikiri mhusika … alikuwa … sana kwa sababu …
- Huenda mwandishi aliandika maandishi haya kwa sababu …

**Tafakari na Jadili**

1. Chagua maandishi ya kusomwa kwa sauti yanayounga mkono malengo ya ufundishaji wa somo lijalo.
2. Jadili aina ya uulizaji na/au mkakati wa majadiliano unaofaa zaidi kufanikisha malengo ya somo husika.
3. Andaa maswali pamoja na majibu yanayolingana ambayo yatatumika kuchochea na kuendeleza majadiliano.

# 7 Maandalizi ya kiakili kwa shughuli za usomaji wa sauti

*Mchakato wa maandalizi ya kiakili unahusisha hatua ya kuhamia kutoka kwenye mpango wa somo wa kimaandishi kwenda kwenye mikakati ya ufundishaji na mbinu za mwalimu atakazozitumia papo kwa papo ili kulifanya somo hilo liweze kufikiwa kwa urahisi, lenye mvuto, na lenye ufanisi kwa kila mwanafunzi mmoja mmoja darasani* (Fuhrman, 2024).

Lemov (2021) anasisitiza umuhimu wa kuwekeza muda wa kutosha katika maandalizi ya somo ili kuongeza kiwango cha ujifunzaji, jambo ambalo linahusu pia upangaji wa vipindi vya kusoma kwa sauti. Kitengo hiki kinatoa muhtasari wa tafiti husika ili kusaidia maandalizi ya vipindi vya usomaji vinavyolenga kuongeza ujifunzaji kwa kiwango cha juu. Kiambatisho cha 2 kinatoa kiolezo kitakachosaidia katika maandalizi ya kipindi cha kusoma kwa sauti.

**Sifa za Uzoefu Bora wa Kusoma kwa Sauti**

Fisher na wenzake (2004) waliwachunguza walimu waliotambuliwa kuwa mahiri katika kusoma kwa sauti kwa wanafunzi, na kubaini kuwa kulikuwa na sifa saba zinazofanana miongoni mwa walimu hao. Sifa hizi zina umuhimu mkubwa wa kuzingatiwa wakati wa kuandaa vipindi vya kusoma kwa sauti, na zinaelezwa hapa chini.

1. *Uchaguzi wa maandishi*
Usomaji wa sauti huwa na ufanisi zaidi unapojumuishwa ndani ya vitengo vya kazi (Lane na Wright, 2007), hivyo maandishi yanapaswa kuchaguliwa ili kuunga mkono mtaala. Kwa kiwango bora zaidi, maandishi yenye changamoto huchaguliwa kwa kuwa uwezo wa watoto wa kuelewa wanachosikia huwa umeendelea zaidi kuliko uwezo wao wa kusoma maandishi. Kama ilivyojadiliwa katika Kitengo cha 2, ni muhimu pia kuzingatia kama matumizi ya maandishi mengi na ujumuishaji wa kazi za kifasihi (*fiction*) yanafaa ili kuongeza upokeaji wa maarifa mapya.

2. *Kusomwa mapema na kufanyiwa mazoezi*
Kusoma kitabu kilichochaguliwa kabla ya somo ni jambo la msingi ili kuufahamu vizuri maandishi. Karatasi ndogo za kunata (*sticky notes*) zilizo na maswali zinaweza kuwekwa katika kurasa mahsusi ili kuonesha maeneo yanayofaa kusimama na kuuliza maswali. Msamiati mpya unaweza kuchaguliwa kwa ajili ya kufundishwa (Fisher n.k., 2004). Maandishi yanapaswa pia kutathminiwa ili kubaini kama wanafunzi wanahitaji kupewa maarifa ya awali ili kuyaelewa (Lewis Hennessy, 2021). Walimu wanapaswa kuandika majibu wanayotarajia kutoka kwa wanafunzi, kwa kuwa mchakato huu unawahamasisha walimu kuweka mawazo yao wenyewe katika maneno, kama ambavyo wanafunzi wanatakiwa kufanya. Hii huwasaidia walimu kutafakari somo na kurekebisha nyenzo za ufundishaji inapohitajika (Lemov, 2021).

3*. Kuweka lengo la kusoma*
Kuweka lengo la kusoma na kulieleza wazi kwa wanafunzi ni jambo muhimu (Fisher n.k., 2004). Lengo hili linaweza kuwa, kwa mfano, kufanya mazoezi ya mkakati fulani wa ufahamu wa maandishi. Wanafunzi wanapoelewa wanachotarajiwa kujifunza, huweza kutanguliza mambo yaliyo muhimu zaidi.

4. *Kuonesha mfano wa usomaji fasaha*
Usomaji fasaha ambapo msomaji anatambua maneno kwa haraka na kwa usahihi na kusoma kwa lafudhi na hisia zinazofaa; ndilo lengo kuu la kusoma (Dougherty Stahl, Flannigan na McKenna, 2020). Kama inavyoonyeshwa katika Mchoro wa 1 (*The Reading Rope*), usomaji fasaha (au usomaji stadi) hutokea pale msomaji anapokuwa mahiri katika stadi zote tofauti zinazochangia usomaji bora. Kusoma kwa sauti kwa wanafunzi hutoa fursa ya kuonesha mfano wa aina hii ya usomaji (Fisher n.k., 2004).

5. *Kusoma kwa uhuishaji na hisia*
Fisher n.k. (2004) walibaini kuwa walimu wenye ufanisi wanaposoma kwa hisia, hutumia ishara za mikono na maelezo ya uso kuwasilisha maana, jambo linalosaidia kuwashirikisha wanafunzi katika hadithi.

6. *Kujadili maandishi*
Kitengo cha 6 cha kozi hii kinatoa maelezo ya kina kuhusu kusaidia (kuskafulidi) majadiliano yanayohusiana na maandishi.

7. *Kusoma na kuandika kwa kujitegemea*
Fisher n.k. (2004) wanapendekeza kuwa watoto wanaweza kushiriki katika uandishi wa jarida wakitumia usomaji wa sauti kama chanzo cha msukumo, au usomaji huo unaweza kuwa kichocheo cha kufanya utafiti kuhusu mada fulani inayohusiana na kitabu.

**Utaratibu wa ufundishaji wa kusoma vitabu vya picha kwa sauti kwa watoto wadogo**

Ili kuongeza manufaa ya kusoma kwa sauti kwa watoto wadogo, McGee na Schickedanz (2007) wanapendekeza utaratibu ufuatao wa ufundishaji unaohusisha kusoma hadithi mara kadhaa:

*Wakati wa usomaji wa kwanza*
Toa msaada wa kujifunza msamiati mpya. Chagua maneno ambayo ni muhimu kwa ufahamu wa maandishi husika na pia kwa kuelewa maandishi mengine. Eleza kwa ufupi maneno haya yaliyoteuliwa mapema kila yanapojitokeza katika hadithi, bila kuvuruga mtiririko wa simulizi (Beck, McKeown na Kucan, 2013). Endapo kitabu hakina istilahi zinazohitaji ufundishaji wa wazi, maneno yenye utata zaidi yanayoweza kutumika kuelezea hadithi kama vile *disaster* au *dramatic* yanaweza kujumuishwa katika mazungumzo wakati wa utangulizi wa kitabu (McGee na Schickedanz, 2007).

*Fikiri kwa sauti*
Ili kujenga ufahamu wa watoto kuhusu hadithi, McGee na Schickedanz (2007) wanapendekeza mwalimu kusimama katika sehemu zinazohitaji msomaji kutoa hitimisho kuhusu kinachoendelea. Mwalimu anaweza kisha kuonesha mawazo yake ya kichanganuzi kwa kusema, *“Ninafikiria kwamba …”*

*Uliza maswali ya “kwa nini?”*
Baada ya kusoma hadithi, mwalimu huuliza maswali ya *kwa nini?* ili kuwahamasisha wanafunzi kutoa hitimisho kuhusu sehemu za hadithi, kwa kuwa watoto wadogo huwa na changamoto katika kutoa hitimisho kutoka kwenye maandishi (McGee na Schickedanz, 2007).

*Wakati wa usomaji wa pili*
Kwa hali bora, usomaji huu hufanyika siku moja au mbili baadaye kwa lengo la kuimarisha uelewa wa watoto kuhusu hadithi kwa kuwashirikisha katika majadiliano ya kina zaidi ya kichanganuzi. Kipindi huanza kwa muhtasari mfupi wa hadithi. Maelezo

mafupi ya msamiati uleule hutolewa tena, lakini maneno ya ziada pia hutambuliwa kwa ajili ya kufundishwa. Uulizaji maswali unakuwa sehemu muhimu zaidi ya kipindi cha usomaji wa sauti, kwa msisitizo kwenye maswali ya kihitimisho na utabiri wa kinachoweza kutokea endapo hadithi ingeendelea (McGee na Schickedanz, 2007).

*Wakati wa usomaji wa tatu*
Kipindi huanza kwa kuwauliza wanafunzi kukumbuka vipengele vya hadithi. Kufikia usomaji wa tatu, lengo ni kuongeza kiwango cha majadiliano ya kichanganuzi ambayo watoto wanashiriki (McGee na Schickedanz, 2007).

**Tafakari na Jadili**

Andika mpango wa somo kwa kutumia kiolezo kilichotolewa katika Kiambatisho cha 2 kwa somo lijalo litakalojumuisha usomaji wa sauti wa maandishi moja au zaidi. Tumia sifa za uzoefu bora wa usomaji wa sauti kama zilivyofupishwa katika kitengo hiki ili kuongoza upangaji wako.

# Kiambatisho cha 1: Matukio ya Somali wa sauti

Matukio ya usomaji wa sauti ni njia ya kufurahisha na kushirikisha watoto katika kukuza upendo wao kwa fasihi na kuendeleza utamaduni wa kusoma. Matukio mbalimbali ya usomaji yanayoandaliwa kila mwaka yameelezwa hapa chini, ambayo yanaweza kutoa msukumo wa kuandaa tukio lako mwenyewe.

*Saa ya Kitaifa ya Kusoma Hadithi kwa Pamoja*
Hili ni tukio la kitaifa la usomaji nchini Australia ambapo shule kote nchini Australia husoma kitabu kilekile cha picha siku moja, kwa wakati mmoja.
https://tinyurl.com/aboutNSS

*Usomaji wa Pamoja wa Kimataifa*
Tukio hili hufanyika kwa kipindi cha wiki sita kwa kutumia kitabu kilichoteuliwa mapema ambacho wanafunzi hukisoma na kukichambua, kwa lengo la kuunda miunganiko ya kimataifa inayohusiana na maandishi hayo kadri iwezekanavyo. Shule huunganishwa na shule nyingine duniani kote kama sehemu ya mradi huu.
https://theglobalreadaloud.com

*Siku ya Kusoma kwa Sauti Duniani*
Hili ni tukio la kila mwaka linaloadhimisha fasihi na umuhimu wa kusoma kwa sauti. Waandaaji wanaweza kuchagua kusherehekea siku hii kupitia michezo ya fasihi, uundaji wa hadithi, au kushirikisha usimulizi wa hadithi na wanafunzi wao. Aidha, mzungumzaji wa kushtukiza (*mystery speaker*) au wazazi wanaweza kualikwa kusoma kwa sauti kwa wanafunzi.
https://www.litworld.org/worldreadaloudday

*Siku ya Kimataifa ya Kitabu cha Watoto*
Ingawa si tukio linalolenga moja kwa moja usomaji wa sauti, limeundwa kuhamasisha upendo wa kusoma miongoni mwa watoto. Vipindi vya kusoma kwa sauti vinaweza kujumuishwa kama sehemu ya shughuli zilizopangwa kwa ajili ya kusherehekea tukio hili.https://www.ibby.org/awards-activities/activities/international-childrens-book-day

*Book Raps*
Hii ni shughuli inayohusisha wanafunzi kujadili na kushirikishana mawazo yao kuhusu kitabu kilichochaguliwa mapema pamoja na wanafunzi kutoka shule nyingine kwa kipindi cha wiki kadhaa. Kitabu hicho kinaweza kuwa riwaya kwa wanafunzi wakubwa au kitabu cha picha kwa watoto wadogo. Kila wiki, mratibu hutoa maswali ambayo wanafunzi wanayajadili na kuyajibu baada ya kusoma hadithi nzima au sehemu yake. Kila darasa huandaa majibu yao kwa maswali hayo, ambayo kisha huwasilishwa kwa madarasa mengine kupitia barua pepe au majukwaa ya mitandao ya kijamii.

# Kiambatisho cha 2: Kiolezo cha Mpango wa Somo la Usomaji Shirikishi

| |
|---|
| Kichwa cha maandishi: |
| Vichwa vya maandishi saidizi (ikiwa yapo) |
| Lengo la kusoma:<br>*Ni kipengele/ vipengele vipi vya The Reading Rope vitakavyolengwa?* |
| Maarifa ya awali:<br>*Je, maandishi yanajenga maarifa ya awali ya wanafunzi? Ikiwa ndiyo, kwa njia gani?*<br>*Je, wanafunzi wanahitaji kupata maarifa ya ziada ili kuyaelewa maandishi? Ikiwa ndiyo, ni maarifa gani?* |
| Msamiati:<br>*Maneno 2-3 yanayohitaji maelezo mafupi yanapokutwa ndani ya maandishi.* |
| Vidokezo vya majadiliano ya kufikiri kwa sauti:<br>*Kabla ya kusoma:*<br>*Wakati wa kusoma:*<br>*Baada ya kusoma*: |
| Maswali ya baada ya kusoma: |

**Marejeo**


Albright, L.K. and Ariail, M. (2005). Tapping the Potential of Teacher Read-Alouds in Middle Schools. *Journal of Adolescent & Adult Literacy*, 48(7), pp.582–591. doi:https://doi.org/10.1598/jaal.48.7.4.

Anderson, P. (2015). *Teaching reading in the early years*. [online] Australian Council for Educational Research - ACER. Available at: https://www.acer.org/au/discover/article/teaching-reading-in-the-early-years#:~:text=Results%20from%20the%20Programme%20for [Accessed 17 Aug. 2024]

Beck, I.L., McKeown, M.G. and Kucan, L. (2013). *Bringing Words to Life, Second Edition*. Guilford Press.

Dougherty Stahl, K.A., Flanigan, K. and Mckenna, M.C. (2020). *Assessment for Reading Instruction*. 4th ed. New York: Guilford Press.

Faddis, T. (n.d.). *Promoting Ongoing Professional Learning Using Text and Discussion Protocols | International Literacy Association*. [online] www.literacyworldwide.org. Available at: https://www.literacyworldwide.org/get-resources/instructional-practices/promoting-ongoing-professional-learning-using-text-and-discussion-protocols?Site=ILA [Accessed 7 Dec. 2023].

Fisher, D., Flood, J., Lapp, D. and Frey, N. (2004). Interactive Read-Alouds: Is There a Common Set of Implementation Practices? *The Reading Teacher*, 58(1), pp.8–17. doi:https://doi.org/10.1598/rt.58.1.1.

Furman, L. (2019). Choral Reading: Say No to Round Robin. [online] Portland, Oregon: International Society For Technology In Education, p.Engaging young readers : practical tools and strategies to reach all learners. Available at: https://ebookcentral.proquest.com/lib/ecu/reader.action?docID=5880794 [Accessed 10 Jan. 2023].

Fuhrman, R. (2024). Beyond Planning: Intellectually Preparing Your Lessons. *Peers and Pedagogy: A Community Blog Focused on Educational Excellence and Equity.* Available at: https://www.learnwithsap.org/peersandpedagogy/beyond-planning-intellectually-preparing-your-lessons/#:~:text=The%20intellectual%20prep%20process%20is,individual%20student%20in%20your%20classroom. [Accessed 21 Jul. 2024].

García, G.E., Sacco, L.J. and Guerrero-Arias, B.E. (2020). Cognate Instruction and Bilingual Students' Improved Literacy Performance. *The Reading Teacher*, 73(5), pp.617–625. doi:https://doi.org/10.1002/trtr.1884.

Kambach, A. and Mesmer, H. (2024). Comprehension for Emergent Readers: Revisiting the Reading Rope. *The Reading teacher*, 77(6). doi:https://doi.org/10.1002/trtr.2315.

Lane, H. and Wright, T. (2007). Maximizing the Effectiveness of Reading Aloud. *The Reading Teacher*, [online] 60(7), pp.668–675. doi:https://doi.org/10.1598/rt.60.7.7. Lemov, D. (2021). *Teach Like a Champion 3.0 : 63 Techniques That Put Students on the Path to College.* 3rd ed. Newark, United States: Jossey-Bass.

Lemov, D., Driggs, C. and Woolway, E. (2016). *Reading reconsidered : a practical guide to rigorous literacy instruction*. San Francisco, Ca: Jossey-Bass & Pfeiffer Imprints, Wiley

Lewis Hennessy, N. (2021). *The reading comprehension blueprint : helping students make meaning from text*. Baltimore, Maryland: Paul H. Brookes Publishing Co.

McGee, L.M. and Schickedanz, J.A. (2007). Repeated Interactive Read-Alouds in Preschool and Kindergarten. *The Reading Teacher*, 60(8), pp.742–751. doi:https://doi.org/10.1598/rt.60.8.4.

Oczkus, L.D. (2012). *Best ever literacy survival tips : 72 lessons you can't teach without*. Newark, De: International Reading Association.

Scarborough, H. (2001). *The Reading Rope* [Image]. *Better Reading Through Science: Using Research-Based Models to Help Students Read Latin Better*. Available at: https://www.researchgate.net/figure/The-Reading-Rope-Scarborough-2001_fig2_282550319 [Accessed 10 Aug. 2024].